
Somo la

# 14 UBATIZO

Kijana huyu Hamid anashangaa. Mwaka uliopita alikabidhi maisha yake kwa Yesu Kristo. Anaendelea vizuri katika Imani yake mpya. Hivi karibuni kuna muumini mwingine alimwambia, "Unapaswa kubatizwa". Hii ilianzisha maswali mengi sana akilini mwa Hamid:




***Hamid***

Hebu tuanze kujibu kila swali la Hamid katika somo letu la leo.

## 'Ubatizo ni nini?'

**1** 'Kwa maana ya kawaida 'Ubatizo' ni kuzamishwa ndani ya maji. Katika Agano Jipya tunasoma namna Yohana Mbatizaji (*Yahya*) alivyobatiza watu katika mto Yordani, akiwemo hata Yesu mwenyewe. Siku hizi wafuasi wa Kristo wanaweza kubatizwa mtoni au bwawani, kwa kuzama majini kwasekunde chache. Njia mbadala ni ile ya kunyunyizia maji kwao.

Huwa tunapitia hatua hii mara moja tu, na huwa hairudiwi katika maisha yetu. Tukio hili huitwa? ______________

## 'Kwa nini nitabizwe?'

**2** Tunabatizwa maana Bwana Yesu aliamuru. Alisema

| |
|---|
| ***"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu".*** (Mathayo 28:19) |

Huu ni mstari muhimu sana. Tafadhali ukariri sasa hivi.

**3** Kwa kutii amri ya Kristo, mtume Petro aliwaambia makutano huko Yerusalemu *"Tubuni mkabatizwe"* (Mdo. 2:38). Siku hiyo watu elfu tatu waliupokea ujumbe wake na kuchukua hatua ya kubatizwa!

Ni sababu gani nzuri kwangu ya kubatizwa? *(chagua jibu moja)*

___ a) kwa sababu nataka kufanya hivyo
___ b) kwa sababu rafiki yangu Mkristo anataka nifanye hivyo
___ c) kwa sababu Bwana Yesu ameniagiza nifanye hivyo

## ‘Ubatizo huonyesha nini?’



Ubatizo ni maalumu sana na ni muhimu. Kulingana na Agano Jipya, ubatizo huonesha kwamba:

A. Mimi ni kiumbe kipya katika Kristo
B. Dhambi zangu zimeondolewa
C. Nimejiunga na jumuia ya Kristo Sasa

Hebu tujifunze kuhusu kweli hizi.

### *A) Mimi ni kiumbe kipya katika Kristo*

**4** Baadhi ya wafu hupatwa na hofu kuzama ndani ya maji wakati wa ubatizo. Usihofu, wakati wa ubatizo watu huzama ndani ya maji tu kwa sekunde chache tu na siyo hatarishi. Lakini ni ishara yenye maana sana kwa kile kilichotokea kwetu tulipomgeukia Kristo. Ni kama utu wetu wa kale unazamishwa ndani ya maji ili kwamba tufufuke tena na utu mpya katika Yesu!

Chora mistari hapo chini ukilinganisha matendo na maana zake:

| *Tendo* | *Maana* |
|---|---|
| a) Kuzama ndani ya maji | 1. Nafufuka tena nikiwa kiumbe kipya katika Kristo |
| b) Kuibuka kutoka majini | 2. Utu wangu wa kale unafishwa |

**5** Hivyo, ubatizo ni ishara ambayo utu wangu wa kale umekwisha na sasa mimi ni kiumbe kipya katika Kristo. Neno la Mungu linasema,

***“Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima”*** (Warumi 6:4)

Ubatizo huonyesha ukweli gani wa kwanza? *(wekea mduara jibu sahihi)*
[ Mimi ni kiumbe kipya katika Kristo/ Mimi bado niko katika utu wangu wa kale, asili ya dhambi]

**6** Mara nyingi wakati wa ubatizo watu huzama majini wakiwa wamevaa nguo zao za kale ikiwa ni ishara ya utu wao wa dhambi. Kisha hutoka majini na kuvaa nguo safi kuonyesha utu mpya katika Kristo.

***Kama ulikwisha kubatizwa, ulikuwa na mihemuko gani ulipotoka majini? Uwe tayari kuzungumzia hili wakati wa majadiliano.***

**7** Siraj kutoka Afrika alimpokea Kristo kutoka kwenye dini ile ile ya kale kama wewe. Hapa anaeleza kwa maneno yake namna alivyojisikia baada ya ubatizo wake:

> “Nilihisi nimekufa katika utu wangu wa kale wenye dhambi, nimeitoa nafsi yangu kwa Mungu na sasa ni mtu mpya. Mimi siyo Siraj ambaye marafiki zangu walimjua, siyo yule yule ambaye Shetani alimjua, bali ni Siraj mpya - aliyesamehewa, aliyezaliwa upya, anayetawaliwa na Roho. Siraji wa kale amekufa, mpya sasa yu hai ndani ya Kristo. Niliibuka kutoka majini nikihisi mimi ni mtu mpya!”

Katika kisanduku hicho hapo juu, ni mara ngapi Siraji ametumia neno ‘mpya’? ___ Yapigie mstari.

**8** Ubatizo huonyesha ukweli gani wa kwanza? Mimi ni mtu _____ ndani ya Kristo

## *B) Dhambi zangu Zimeondolewa*



**9** Matendo ya Mitume 22:16 inatuambia kuhusu kweli ya pili kuhusu ubatizo: "*ubatizwe, ukaoshe dhambi zako*".

Kulingana na mstari huu, ubatizo huonyesha kweli gani? (*chagua moja*)

___ a) Mimi ni mtu mpya katika Kristo
___ b) Dhambi zangu zimeondolewa

**10** Kama tunavyojua kutokana na uzoefu wetu wenyewe, kutawadha (*wudu*) au hata kuoga mwili mzima (*ghusal*) haitoshi kuondoa dhambi zetu. Maji yanaweza kusafisha tu nje ya miili yetu, hayawezi kusafisha mioyo na dhamiri zetu.

Hata hivyo, ubatizo ni ishara ya nje yenye nguvu ya usafi wa ndani ambao Kristo huufanya ndani ya mioyo yetu. Alikufa msalabani ili kuliwezesha hili. Soma 1 Yohana 1:7 *(kwamba 1 Yohana ni kitabu kingine cha Biblia tofauti na injili ya Yohana. Tazama kwenye orodha yako ya Yaliyomo).*

Kulingana na 1 Yohana 1:7, ni nini kinachotusafisha dhambi zote? ______________________

**11** Mtume Petro, aliyebatiza watu wengi sana wakati wa uhai wake, pia aliandika kuhusu ubatizo katika 1 Petro 3:18-22. Kifungu hiki huwa siyo rahisi kukifafanua. Lakini hoja kuu ni:

- Wokovu wetu ni kupitia mateso ya Yesu (mstari 18) na ufufuo (mstari 21)
- Maji ni alama ya wokovu huu kwetu (mstari 21) kama ilivyokuwa kwa Nuhu (mstari 20)

Ni tukio gani linalonikumbusha kwamba dhambi zangu zimeondolewa?

___ a) ubatizo wangu ___ b) hija yangu ___ c) mazishi yangu

## *C) Nimejiunga na jumuia ya Kristo*



**12** Kwa kubatizwa tunatangaza hadharani kujiunga na jumuia ya waamini wa Kristo ulimwengu kote (*ummah* wa Kristo). Sisi ni wanaume na wanawake kutoka katika tabaka mbalimbali, lakini wote tumeungana *"Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwii mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi zote tulinyweshwa Roho mmoja."* (1 Wakorintho 12:13).

Ubatizo huonyesha ukweli gani wa tatu? Nimejiunga na jumuia ya _____________

**13** Ubatizo siyo kitu cha faragha kwa ajili yako tu, bali unahusisha jumuia nzima ya waamini. Watashuhudia tukio lako la ubatizo, na mwishowe wanaweza kutumia maneno kama haya ili kukukaribisha:

> "Tunakukaribisha katika familia ya Bwana. Sisi kwa pamoja tu sehemu ya mwili wa Kristo, sisi kwa pamoja tu watoto wa Baba wa Mbinguni, sisi kwa pamoja ni warithi wa ufalme wa Mungu. Tunakukaribisha sana."

***Tuna neema iliyoje kukaribisha na 'watu waliochaguliwa na Mungu'! Sitisha sasa umshukuru Mungu kwa ndugu zako walio ndani ya Kristo.***

**14** Ubatizo huonyesha kweli tatu zipi? *(jaza nafasi zilizoachwa wazi)*

a) Mimi ni mtu______katika Kristo

b) __________ zangu zimeondolewa

c) ___________ jumuia ya Kristo

Hamid amefurahi sana kujifunza kweli hizi. Baadaye anauliza:

## ‘Je! Ubatizo ni muhimu?’

**15** Kwa namna moja siyo muhimu kwa wokovu, maana tunaokolewa kwa kumtumaini Kristo na siyo kwa maji. Lakini bado, ubatizo ni amri ya Kristo! Na kama tulivyokwisha kuona, ni ishara muhimu sana ya kuwa watu wake katika kanisa lake. Hivyo ni muhimu kubatizwa, wakati ukiwa sahihi.

a) Katika tamaduni nyingi, ukiona pete ya ndoa kwenye kidole cha mtu, hiyo huonyesha nini? ____________________________

b) Pete siyo muhimu sana kwa ajili ya kuoa au kuolewa, lakini katika baadhi ya tamaduni ni ishara muhimu kwamba mtu huyo ni wa mwingine? ______________

c) Vivyo hivyo, ubatizo wetu ni alama muhimu ya kwamba sisi ni wa nani? _____________

**16** Kupitia ubatizo tunaonyesha tunafurahi kuwa tu mali ya Yesu Kristo. Na tunafurahi kuwaambia ndugu zetu walio katika Kristo. Yawezekana utaombwa ‘kutoa ushuhuda wako’ kuhusu ubatizo wako. Hii ina maana kwamba ueleze kwa kifupi tu ukimwambia kila mtu namna Yesu Kristo alivyobadilisha maisha yako.

Hebu tujaribu sasa hivi. Waza kwamba siku moja unatoa ushuhuda wako kwenye ubatizo wako. Kiongozi atakapouliza “Kristo amefanya mabadiliko gani katika maisha yako?”, utasema nini. *Andika kile utakachokisema na uwe tayari kwa majadiliano. Kama unataka, angalia ulichoandika katika somo la 2 swali la 15. Lakini andika hapa kwa kina zaidi.*

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________


________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

**17** Hali ya Salma bado haimruhusu kubatizwa. Ni ushauri gani mzuri wa kumpa, a) au b)?

___ a) ‘Usijisumbue, ubatizo siyo muhimu’

___ b) ‘Ubatizo ni muhimu sana, hivyo endelea kumwomba Mungu atoe kibali kwa ajili ya ubatizo wako ufanyike kwa wakati sahihi’



## ‘Nibatizwe lini?’

**18** Baadhi ya Wakristo wanakushawishi upate ubatizo mara unapompokea Kristo. Wengine wanasema ni vizuri kusubiri kidogo mpaka imani yako iimarike. Sikiliza ushauri wao, lakini sikiliza ushauri wa Roho wa Mungu pia. Mungu mwenyewe atakuongoza katika hatua hii muhimu. Wakati ukifika, utasikia moyoni mwako.

Usiruhusu watu wakukimbize ili upate ubatizo wa haraka kama hujawa tayari. Kama Mungu anakwambia sasa ni muda sahihi, usibaki nyuma.

Ni matendo gani hayo hapo chini ni mema? *(chagua mawili)*

___ a) kusikiliza ushauri wa waamini wenye busara wanaokujali
___ b) acha kubatizwa kwa sababu unaogopa matokeo yake
___ c) unafikiri siyo muhimu kubatizwa
___ d) batizwa pale unahisi Mungu anakwambia kufanya hivyo

**19** Waamini wenye busara wanakujali na watakupa ushauri mzuri kuhusu ubatizo. Lakini kuna waamini ambao hawana busara katika kufanya mipangilio ya ubatizo, na kuna baadhi ya viongozi wa kanisa ambao hutumia ubatizo ili kuvumisha jina lake. Hivyo tafuta mtu unayemwamini ili akusaidie kufanya mipangilio yako ya ubatizo.

Kama unamfahamu atakayekupatia ushauri wa busara kuhusu ubatizo wako, weka alama ya vema kwenye kisanduku hiki ☐. Kama hujui mtu atakayekufaa, mwulize mshauri wako.

**20** Tulifikiria hapo awali maana ya ubatizo kwetu waamini. Lakini una maana gani kwa ndugu zetu wasio Wakristo? Kwao ni ishara ya wazi kwamba tunajitenga nao, inawasababishia maumivu na aibu.

Tufanye ubatizo kwa namna gani?


___ a) Kwa hofu, tukiwa na mashaka kuhusu usalama wetu
___ b) Kwa makini, kwa upendo kwa familia zetu

**21** Utatoa ushauri wa namna gani kwa muumini ambaye mkewe au mmewe bado siyo Mkristo? Je, muumini huyo abatizwe mara, au asubiri akitumaini mwenza wake atakapomwamini Kristo? *Zingatia mawazo yako na uwe tayari kwa majadidiliano.)*

______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________

**22** Kwa sababu ya ndugu zetu wasio Wakristo, inashauriwa ni vizuri kuwa makini na kuchukua tahadhari. Ni tahadhari zipi unazoziwaza, kwamba ubatizo wetu hautasababisha hali ya kufedheheka kwa ndugu zetu? *(Zingatia mawazo yako na uwe tayari kwa majadiliano.)*

______________________________________________________________
______________________________________________________________



**KAZI YA KUFANYA**

Kama bado hujabatizwa, nenda ukazungumzie hilo na mtu uliyemtaja katika swali la 19. Pata ushauri wao kuhusu lini na namna unavyopaswa kubatizwa. Pia, omba ushauri kutoka kwa Bwana.

## MARUDIO

1 Andika mstari wa kukariri: "Basi, enendeni mkawafanye mataifa kuwa wanafunzi, ____________________________________________________________ (Matthew ___ : ___)


2 Tulijifunza kwamba ubatizo wangu ni ishara ya mambo matatu.Ni mambo gani hayo?
a) 'Mimi ni ______________'
b) ' __________ zangu _______________'
c) 'Nimejiunga na _____________ Kristo.'

3 Kubatizwa kuna umuhimu gani?

___ muhimu sana ___ siyo muhimu

## SOMO LA 13 MAJIBU

1 soma mstari ili kupata majibu
2 jibu binafsi
3 Msiogope
4 Hapana
5 B
6 Yusufu
7 Msiogope
8 uwe tayari kwa majadiliano
9 jibu binafsi
10 kariri mstari
11 Mungu
12 andika mstari kama ulivyoukariri kichwani
13 uwe tayari kwa majadiliano
14 b)
15 kwa hofu
16 c)
17 kwa ajili ya majadiliano
18 a) na b) ni sahihi
19 c)
20 Hapana




## SOMO LA 14 MAJIBU

1 ubatizo
2 kariri mstari
3 c)
4 a) 2 b) 1
5 Mimi ni kiumbe kipya katika Kristo
6 mwitikio binafsi
7 4
8 mpya
9 b)
10 damu ya Yesu
11 a)
12 waamini wa Kristo ulimwengu kote
13 tulia na mshukuru Mungu
14 a) mpya; b) dhambi;
c) kuunganishwa
15 a) kwamba mmeoana tayari
b) mume au mke wako
c) Kristo
16 uwe tayari kutoa ushuhuda wako kwenye kikundi
17 b) ubatizo ni muhimu sana
18 a) na, d) ni nzuri
19 weka alama ya vema ndani ya kisanduku kama unamfahamu mtu anayeweza kukushauri
20 b)
21 kwa ajili ya majadiliano
22 kwa ajili ya majadiliano